GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. **252** Dhl/Hijjah-Muharram **1446-7** AH Juni– **2025** Ihsan **1404** HS BEI TSH 800/=

Hija au kuhiji Makka



Na. Sufi M.R. Bangalee M.A.
Imetafsiriwa na Sheikh. Shabani Athumani Shunda.

Hija au kuhiji Makka, ambayo ni moja ya nguzo za Uislamu, ni wajibu juu ya kila Muislamu kuitekeleza walau mara moja katika maisha yake. Inakuwa ni lazima tu chini ya hali fulani, kama vile afya ya mwili, uwezo wa kifedha, usalama katika njia, na nyenzo za usafiri.

Miezi mitatu mitukufu ya Shawwal, Dhū al-Qa'dah, na Dhū al-Hajjah ni msimu uliowekwa wa kuhiji. 'Umrah, au hijja ndogo, inaweza kufanywa wakati wowote, isipokuwa katika msimu wa Hajj. Inatofautiana na Hijja katika baadhi ya sura zake za utekelezaji, au Hija sahihi.

Ni muhimu kwa Haji au mwenye kuhiji, kufunga safari hii tukufu kwa madhumuni na nia ya dhati ya kuhiji. Anapofika Miqaat, vituo vilivyowekwa ambavyo viko umbali wa maili tano au sita kutoka Makka, kwenye barabara mbalimbali zinazoelekea mji mtakatifu, hujaji baada ya kutawadha na kuswali avue nguo yake ya kawaida na achukue Ihram au vazi la hujaji, ambalo lina shuka mbili zisizo na mshono, moja ambayo shuka itafungwa kiunoni na nyingine itatupiwa mabebani. Wakiwa katika hali ya ihram, Haji lazima ajiepushe na mambo ya dunia. Hatakiwi kunyoa hata kidogo, wala asipunguze kucha zake, wala asitie mafuta kichwa chake, wala asiwinde. Ni lazima ajitose moja kwa moja kwa ajili ya sala na kumkumbuka Mungu. Miundo na misemo ya maneno ambayo Haji anatakiwa kurudia mara kwa mara ni kama ifuatavyo:

لَبَّيْكَ ٱللَّٰهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ ٱلْحَمْدَ وَٱلنِّعْمَةَ لَكَ وَٱلْمُلْكَ لَا شَرِيكَ لَكَ

Labbaik, Allahumma Labbaik, Labbaik La Sharika laka Labbaik. Inn-al-

UK. 03

JAMIA AHMADIYYA TANZANIA WAFANYA ZIARA YA UTALII NA MAFUNZO.

Moja ya program za kila mwaka katika chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya ni kufanya ziara za kutembelea maeneo mbalimbali muhimu ili kupata fursa ya kujionea na kujifunza mambo mbalimbali ya

UK. 04

HEKIMA YA DHABIHU Asemavyo Masihi aliyeahidiwa[as] UK. 08

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

UVUMILIVU

Kwa masikitiko makubwa, uvumilivu imekuwa bidhaa adimu duniani. Simama kutoa maoni yako na kabla hujafika mbali unavutwa shati na kuambiwa kukaa chini kama utakuwa umenusurika kuzabwa makofi. Ukiwa na wazo tofauti au kutofautiana na wengine wewe ni adui mkubwa na unatakiwa utoswe baharini haraka iwezekanavyo. Haya yote yanatokea kwa sababu ya kutozingatia mafundisho ya dini Tukufu ya Islam.

Kabla ya Islam, bidhaa hii haikuwepo kabisa, historia inatusaidia kuthibitisha hoja hii Byzantine na Wafarsiy falme hizi mbili hazikuwa na uvumilivu wa kidini. Hawakuwa na uhuru kabisa wa kuabudu. Wale wote waliokuwa na maoni tofauti na Mfalme walihesabiwa ni maadui. Na ilikuwa vigumu kuishi chini ya utawala wao. Huko Syria Wanestori ilibidi kuhama kwa sababu hapakuwepo na uhuru wa kuabudu.

Islam imeleta mapinduzi makubwa. Kimsingi Islam imepinga kuabudu masanamu. Inasisitiza juu ya umoja wa Allah na ukweli wa Dini zilizofunuliwa. Na huu ndio msingi wa Islam. Manabii wote wanaheshimiwa na hakuna kuwatofautisha. Qur'an Tukufu inasema; "Semeni: Tumemwamini Allah nay ale tuliyoteremshiwa na yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu na Ismaili na Isihaka na Yakubu na wazao wake, na pia yale aliyopewa Musa na Isa na yale waliyopewa Manabii kutoka kwa Mola wao; hatutofautishi baina ya mmoja kati yao, na sisi tumejitupa Kwake" (Qur'an Tukufu Sura 2:137). Na Waislam wamekumbushwa kwamba wap wana Dini yao, na ninyi mna Dini yenu, msiwatukanie miungu yao, wasije wakamtukana Mungu wenu wa kweli kwa ujinga pasipo kujua. Ilitokea Sahaba mmoja wa Mtukufu Mtume[saw] alibishana na Myahudi mmoja kuhusu ubora wa Mtukufu Mtume[saw] juu ya Nabiii Musa[as], ambapo yule Myahudi alichukia na kudai hapana bali Nabii Musa ndiye bora. Mabishano yao yalipofikishwa kwa Mtukufu Mtume[saw], yeye aliamulia kesi yao kwa kusema; "Usinitukuze juu ya Musa" na mabo yote yakawa yameisha. Mtukufu Mtume[saw] alipohamia Madina na kuwa mtawala wa hapo, yeye alifanya mkataba wa Amani baina ya Waislam na Mayahudi na kwenye mkataba huo uhuru wa kuabudu ulizingatiwa kikamilifu. Na pia ilikuwa ni desturi ya Mtukufu Mtume[saw] kwa mambo yale ambayo Qur'an Tukufu ilikuwa bado haijatoa mwongozo rasmi, yeye alikuwa akitumia sheria ya Mayahudi. Kutofautiana ni jambo ambalo Mtukufu Mtume[saw] alikubaliana nalo na alisema; "Kutofautiana kwa Maulamaa wangu ni rehema". Wakristo wa Najilani waliruhusiwa kufanya ibada yao katika Msikiti Mtakatifu wa Madina. Makanisa hayakubomolewa. Maaskofu hawakuondolewa katika ofisi zao. Masanamu yao na misalaba yao haikuguswa. Maoni ya viongozi wa Kanisa katu hayakuingiliwa. Masahaba waliombwa kuwalinda Wakristo na Makanisa yao. Waliodhamiria kwenda kutembelea sehemu zao takatifu waliruhusiwa. Akina mama walioolewa na waislam waliendelea kufuata dini zao. Katu Makanisa hayakuvunjwa ili kujenga Msikiti au nyumba kwa ajili ya Waislam. Je kuna uvumilivu kuliko mapatano ya Hudaibiyyat. Makafiri wa Makka walipokataa kuweka neno "Rasuulullah" kwenye Mkataba, Mtukufu Mtume[saw] alikubaliana nao. Muislam wa Makka alizuiliwa kwenda Madina kuungana na Waislam wenzake, lakini Muislam wa Madina akienda Makka hakuruhusiwa kurudi Madina.

Dawa ya uvumilivu, imetolewa na Islam. Ni busara kuitumia ili kutibu maradhi yanaisibu dunia kwa hivi sasa. Na katu tusisahau ushairi wa Mshairi 'Simba wa Lumona'; "Kula Mziwanda kula, kula upate afya".



QUR'AN TUKUFU

Umekwisha isadikisha ndoto. Kwa yakini hivi ndivyo Tuwalipavyo watendao mema.
Bila shaka (jambo) hili ni jaribio la bayana. Na Tukamkomboa kwa dhabihu kubwa. Na Tukamwachia sifa kwa watu wa baadaye.

قَدْ صَدَّقْتَ الرُّؤْيَا ۚ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ.
. إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ الْبَلَاءُ الْمُبِينُ
وَفَدَيْنَاهُ بِذِبْحٍ عَظِيمٍ .
وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ



NUKUU YA HADITHI

إني عند الله في أم الكتاب لخاتم النبيين وإن آدم لمنجدل في طينته، وسأنبئكم بتأويل ذلك: دعوة أبي إبراهيم، وبشارة عيسى قومه، ورؤيا أمي التي رأت أنه خرج منها نور أضاءت له قصور الشام،.
(المحدث: شعيب الأرناؤوط في تخريج المسند لشعيب – ١٧١٦٣ الراوي: العرباض بن سارية)

Tafsiri: kwa Yakini mimi ni Khatam un nabiyyin mbele ya Allah Mtukufu katika ummu ul Kitab ilhali Adam alikuwa baado kuchanganywa udongo wake, nami nitawaelezeni ukweli wake. Mimi ni mwito wa babangu Ibrahim. Na bishara ya Issa kwa watu wake. Na ndoto ya mama yangu, aliyoiona kwamba Nuru imetoka kwake na ngome za Syria zilinga'a kwayo.



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

"Kwa hakika kulikuwa na siri kubwa ndani ya siku hiyo kwamba, dhabihu , aliyoipanda mbegu yake Ibrahim a.s. kwa siri, Mtume s.a.w. alionyesha mazao yake ya kudumu. Hazrat Ibrahim a.s.hakusita katika kumchinjia mwanaye kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Kulikuwa na somo ndani yake kwa siri kwamba mtu awe wa Mungu kwa pande zote na mbele ya amri ya Mungu, uzima wake, kizazi chake,ndugu zake na damu ya wapenzi wake, ionekane hafifu. Katika enzi za Mtume s.a.w.,aliyekuwa mfano kamili wa kila mwongozo uliotukuka, dhabihu ya namna gani ilitolewa? Pori zimejaa na damu kana kwamba mito ilitiririka na damu. Wazazi waliwaua Watoto wao, na Watoto waliwaua wazazi nao walikuwa wanafurahi kwamba kama wanasagwa katika njia ya Mwenyezi Mungu na kukatwa vipand vipande basi itakuwa raha kwao." (Malfoozat.J.1.u.k.327 chapa ya 1988)
Nukuu ya Masih Aliyeahidiwaas

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

Hija au kuhiji Makka

Kutoka uk. 01

Hamda Wan-Ni'mata Laka wal-Mulk, La Sharika Lak.

Tafsiri: "Nimekuitikia Ee Mola, Mimi hapa, Mimi hapa, Huna mshirika wako nakiri. Hakika Sifa zote njema na neema ni zako, na ufalme. Hana mshirika wako." Baada ya kuwasili Haram - eneo takatifu lililo maili chache pembezoni mwa mji wa Makka, wakati Haji anaona Ka'ba kwa mara ya kwanza, anatakiwa kufanya maombi kwa umakini kwani huo unachukuliwa kuwa wakati maalum wa kukubaliwa maombi. Kubusu Jiwe Jeusi ambalo lipo katika kona ya Kusini-mashariki ya nyumba ya Mungu hutimiza ibada maalum inayofuata, baada ya hapo Haji hufanya mizunguko saba kuzunguka nyumba takatifu, kila mzunguko akilibusu Jiwe Jeusi. Umati mkubwa unapozuia kuifikia, ishara hufanywa kulielekea kwa mkono, ambao hubusiwa badala yake. Hii inaitwa Tawaf au kuzunguka Ka'ba, mwishowe Haji anatakiwa kusali ndani ya eneo la nyumba tukufu akiwa amesimama nyuma ya Maquam-i Ibrahim, mahala pa Ibrahim.

Hujaji huelekea kwenye vilima vya Safa na Marwa. Kwanza akipanda mlima wa Safa, huku anasoma Takbir au "Allah u Akbar", huku uso wake ukielekea Ka'ba. Kisha anashuka na kuanzia Safa, anakimbia mara saba kati ya vilele viwili. Hii inaitwa Sa'yy, au kukimbia, baada ya hapo, msafiri huyu kuelekea kwa Mwenyezi Mungu hukaa Makka akiwa na vazi laka kihujaji, hadi tarehe nane ya Dhū al-Hajjah. Siku hiyo anakwenda Mina, sehemu ambayo ni maili tatu kutoka Makka. Atawasili hapo kabla ya saa sita mchana na atakaa usiku kucha.

Asubuhi ya siku ya tisa mara baada ya sala ya alfajiri, Haji huelekea Arafat, uwanda ulio umbali wa maili sita kutoka Mina. Anapofika kwenye bonde la Namrah, hujaji anasali sala yake ya adhuhuri na ya alasiri kwa pamoja kisha anaingia Arafa na kubaki humo hadi kuzama kwa jua. Kukaa huku huko Arafat hutimiza sehemu kuu ya ibada za Hajj.

Hujaji anatakiwa ajishughulishe na sala na kumbukumbu za Mungu pekee. Baada ya jua kuzama, Haji anaondoka kutoka Arafat na kwenda Muzdalifa sehemu ya katikati kati ya Arafat na Mina, ambako anapitisha usiku kwa kufanya ibada.

Siku ya kumi ya Dhū al-Hajjah, baada ya sala ya alfajiri, hujaji hutembelea Msikiti mtukufu wa Masharul-Haram na kukaa muda kidogo katika sala. Hutoka hapo kabla ya kuchomoza kwa jua, Haji anakwenda Mina ambako kuna nguzo tatu tofauti zinazoitwa Jamrat al Aqabah, Jamrat al-Wusta, nguzo ya kati, na Jamrat al-'Ula, nguzo ya kwanza au ndogo. Hapo Haji hufanya ibada iitwayo Ramiul-Jimar au kurusha mawe. Anarusha vijiwe saba kwenye Aqabah, kila mara akisoma "Allah u Akbar -Mwenyezi Mungu ni Mkuu." Wakati huo, anaacha kukariri maneno **"Labaika Allahummah - Ee Mola, Mimi hapa"** ambayo alianza wakati wa kuvaa vazi la Hija. Ibada hii ikiisha, hujaji anatoa dhabihu ya Ei'd-ul-Adha, ambayo maelezo yake tayari yametolewa. Utoaji wa dhabihu unaashiria hitimisho la ibada muhimu za Hija. Haji sasa ananyoa kichwa chake, anakata kucha, anavua Ihram yake au vazi la Hija, anaoga na kuvaa tena vazi lake la kawaida. Kinachofuata baada ya haya, Haji anatakiwa kuitembelea Ka'ba na kufanya mzunguko wa kuizunguka na kama hakuweza kufanya mzunguko wa Safa na Marwa hapo awali, lazima aifanye sasa hivi. Kwani bila kufanya haya, Hijja isingetimia. Kisha aelekee Mina na abakie huko mpaka siku ya kumi na tatu ya Dhū al-Hajjah. Wakati wa kukaa kwake Mina, lazima afanye ibada za kurusha mawe kwenye nguzo kila siku baada ya adhuhuri na atumie muda wake wote katika sala na kumbukumbu za Mwenyezi Mungu.

Katika siku ya kumi na tatu, hujaji hufanya ziara yake ya mwisho huko Ka'ba na hufanya mzunguko wake wa kuaga wa nyumba tukufu baada ya kuhitimisha sala yake na hivyo kukamilisha Hija yake. Haji sasa yuko huru kwenda apendapo.

Matendo yafuatayo yanachukuliwa kuwa yenye thawabu: kufanya maombi ikiwa uso, kifua, na tumbo vimegusa ukuta karibu na kona ambapo limewekwa Jiwe Jeusi, na kunywa maji ya kisima cha Zamzam.

Kufanya ziara kwenda kwenye mapango ya milima ya Hira na Thaur, na kwenye Bonde la Abu Talib.

Kusali katika Masjid-ul Haram, Msikiti Mtakatifu wa Makka, Ni desturi ya kichamungu kwa wale mahujaji wanaomudu kufanya hivyo, na kufanya ziara katika mji mtakatifu wa Madina, lilipo kaburi la Mtume Mtukufu Muhammad (sa).

Hekima ya Hajj

Ibada na matendo ya Hajj si maonyesho matupu na yasiyo na maana. Yana maana za kina za ndani za kiroho. Kama vile roho haiwezi kuwepo bila mwili na kokwa haziwezi kuwepo bila ganda, vivyo hivyo, thamanina kweli za kiroho na uzoefu haviwezi kupatikana bila aina ya maonyesho ya vitendo vya nje vya ibada. Katika macho ya Waislamu wa kweli, Hija ni batili na haijaswihi isipokuwa mpaka kila kitendo kilichopangwa kufanyika kiwe kinaambatana na na hali ya roho wakati husika.

Neno Hajj katika lugha ya kiarabu maana yake halisi ni **Qasd** au matamanio na katika umuhimu wake wa kiroho, linaashiria safari kutoka kwenye ulimwengu huu wa kimwili hadi kwa Mungu, ambayo ina maana ya utambuzi na kuungana naye.

Kwenda hijja Makka ni ishara ya heshima inayoonyeshwa mahali ambapo mapenzi ya Mwenyezi Mungu yalidhihirika na hutumika kuwakumbusha waaminio matukio haya. Inakumbusha kisa cha Hazrat Ismail (sa) na Hazrat Hajira (as) walioachwa jangwani na Hazrat Ibrahim (as), na jinsi wale wanaojitolea mhanga katika njia ya Mwenyezi Mungu wanavyolindwa na kuheshimiwa.

Hii inamtia moyo msafiri kuwa na imani hai katika uwezo na uweza wa Mungu. Anajipata karibu na mahali palipowekwa wakfu kwa ibada ya Mungu Mmoja, wa Kweli tangu zamani. Na anakuja kupata uzoefu wa ushirika wa kiroho na wale ambao kwa karne nyingi wameunganishwa kupitia upendo na kumkumbuka Mwenyezi Mungu, ambaye anajihesabu miongoni mwao.

Hija inamzoeza mwislamu kuondoka nyumbani kwake, kuteseka kujitenga na marafiki na jamaa zake, na kupitia taabu za safari hiyo ngumu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kusudi kuu la kuhiji Makka ni utimilifu wa dhamira ya usawa na udugu wa wanadamu. Wakiwa wamevalia mavazi sare, msongamano mkubwa wa mahujaji hujenga mwonekano wa kuvutia. Humo mfalme hawezi kutofautishwa na mkulima wa kawaida. Hapo mfalme anafanywa kutambua kwamba yeye si bora kuliko mtu maskini zaidi katika mtaa. Pale mtumishi mnyenyekevu anafanywa kuhisi kwamba yeye si duni kuliko mfalme mkuu zaidi. Hakika ni chuo kikuu cha udugu wa ulimwengu wote.

T. W. Arnold anasema: "Lakini juu ya yote ndani yake ni umuhimu wake mkubwa katika historia ya kimisionari ya Uislamu-huamuru mkusanyiko wa kila mwaka wa waumini wa mataifa na lugha zote, wanaokusanywa pamoja kutoka sehemu zote za dunia kusali katika mahali patakatifu (Ka'ba) ambapo nyuso zao zimeelekezwa katika kila saa ya ibada ya faragha katika nyumba zao za mbali. Hakuna mtu mwenye akili timamu wa kidini ambaye angeweza kuwa na manufaa bora zaidi ya kukazia akilini mwa waaminio hisia ya maisha yao ya kawaida na ya udugu wao katika kifungo cha imani.

Hapa ni tendo kuu la ibada ya kawaida, ambapo watu weusi wa Pwani ya Magharibi ya Afrika hukutana na Mchina kutoka Mashariki ya mbali; na hakimu mwenye hadhi na hekima kutoka katika ufalme wa Kiuthmani anamtambua ndugu yake Mwislamu kutoka katika kisiwa cha mwitu kutoka mwisho wa mbali wa Bahari ya Malayan. Wakati huo huo katika ulimwengu wote wa KiMuhammad nyoyo za waumini huinuliwa kwa huruma na ndugu zao waliobahatika zaidi waliokusanyika pamoja katika mji mtakatifu (Makka) kama katika nyumba zao wenyewe, wanasherehekea sikukuu ya 'Eid-ul-Adha au (kama inavyoitwa Uturuki na Misri) sikukuu ya Bayram'. **(The Preachings of Islam by T. W. Arnold, p. 338.)**

JAMIA AHMADIYYA TANZANIA WAFANYA ZIARA YA UTALII NA MAFUNZO.

Kutoka Uk wa 1..

muhimu katika jamii. Mwaka huu program hiyo ilifanyika mnamo siku ya Alhamisi ya tarehe 24/04/2025 na eneo lililotembelewani Magadu Ofiicers Club. Eneo hili linamilikiwa na Taasisi Muhimu kabisa katika serikali yetu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania yaani jeshi la wananchi wa Tanzania. Lililopo umbali wa takribani kilomita



kumi kutoka chuo cha Jamia Ahmadiyya Tanzania. Wanafunzi, waalimu wote walipata fursa hiyo adhiimu ya kutembelea eneo hilo. Safari ilianza majira ya 3 asubuhi na kurejea saa 12:00 jioni salama salimini Alhamdulillah. Wakiwa huko vijana (wanafunzi) na waalimu walishiriki katika michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, mpira wa wavu n.k. Amma watoto (Atfal na Nasrat) nao walipata burudani zao za



kubembea n.k. Pamoja na mambo mengine wanachuo pia walipata fursa ya kutembelea vitengo mbalimbali ikiwemo makumbusho ya wapigania uhuru wa Afrika Kusini n.k baada ya yote hayo, wanachuo walipata chakula cha mchana na kisha walisali sala za Adhuhuri na Alasiri na kumaliza ratiba yao.

MAISHA YA MOHAMED IQBAL DAR (1944 – 2025)

Kutoka Uk 11..

Hata alipokuwa Uingereza aliweza kutuma zawadi kwa ndugu na jamaa mbalimbali. Nikiwa naandika Makala haya Sheikh mmoja wa Jamaat alijitokeza na kutoa ushahidi wake kuwa aliwahi kupokea zawadi ya suti mpya kutoka Uingereza kwa Bw. Mohammed Iqbal Dar, mwandishi wa Makala haya pia ni shahidi wa kupokea zawadi ya suti mpya nzuri kutoka kwa Bw. Mohammed Dar.

Msikiti wa pili kujengwa nchini baada ya ule wa Tabora ‘Al-Fazal’ uliofunguliwa mwaka 1944 ulikuwa ni ule uliofunguliwa katika mji mkuu wa siku hizo Dar es salaam na kupewa jina na Khalifatul Masih –II (ra) ‘Masjid Salaam’. Kama ilivyokuwa Al-Fazal, Masjid Salaam ulitokana na juhudi za Wanajamaat ambao walitafuta kiwanja mahali palipodharauliwa na kuitwa ‘Mchafukoge’. Juhudi hizo za kupata kiwanja cha Msikiti huo zinanasibishwa na Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima. Hivi leo hakuna Msikiti ulio mahala pazuri na katikati ya mji kama ulivyo Masjid Salaam. Msikiti huu ulifunguliwa na Maulana Sheikh Mubarak Ahmad mwaka ule wa vuguvugu la uhuru nchini na uhuru wa Ghana mwaka 1957. Hali ya uchumi ilikuwa ngumu sana na Wanajamaat wenye uwezo walikuwa wachache. Katika hali hiyo ngumu Dr. Tufail Ahmad Dar wa Morogoro na Rais wa Jamaat hiyo ya Morogoro alitoa mchango wa Tsh.21,000/= hizo zilikuwa pesa nyingi sana kwa wakati huo. Na jina lake liliandikwa kwenye ukuta wa Msikiti ikiwa ni kumbukumbu kwa vizazi vijavyo kujua ni kwa jinsi gani Wanajamaat waliopita walivyojitolea kwa ajili ya maendeleo ya Jamaat ili nao pia wawezekuiga mwenendo huo wa kutanguliza dini juu ya dunia. Mwenendo huo wa kujenga Misikiti ameurithi Bw. Mohammed Iqbal Dar. Yeye katika agizo lile la ‘Fasta bikul khairat’ amekwenda mbele zaidi na kujenga Misikiti ifuatayo; Manyoni, Kitumbili na Kinyeto mkoani Singida, Mikese Mkoani Morogoro, Lindi Mjini –mkoani Lindi.

Msikiti wa Manyoni uko njiani kabisa na kivutio kikubwa. Msikiti huu umepambwa vizuri kwa maua. Kazi hii nzuri imefanywa na Mwalimu Maulidi Issa Mchana ambae wakati huo alikuwa Afisa wa Elimu wa Wilaya ya Manyoni. Wakati wake wa mapumziko aliacha shughuli zote na kuweza kurembesha nyumba ya Allah. Na ikumbukwe aliyekuwa akifanya kazi ni Afisa Elimu Wilaya ambaye kidunia ni mtu mkubwa sana. Mwalimu Maulidi ambaye alipojiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya aliahidi kutanguliza dini juu ya dunia. Hakujali heshima za duni za uongo na kweli, yeye daima alitafuta heshima na radhi ya Allah.

Ni neema kubwa unapojaaliwa kuacha nyuma watotowanaoendelezamema uliyoyaacha. Na hiyo hasa ndiyo maana ya Sadakatul jaaria. Kuendelea kuvuna yale uliyoyapanda jana. Kwa hilo Dr. Tufail Ahmad Dar amefanikiwa sana, kwani Bw. Mohammed Iqbal Dar amefuata mwenendo wa baba yake sawa na mifano ambayo tumeibainisha. Na hii inatupatia somo kubwa kwamba sote tujitahidi kuwalea watoto wetu katika malezi bora ili kesho waje kubeba majukumu ya kutumikia dini na viumbe wa Allah.

MAJIBU YA BAADHI ZA SHUTUMA/PINGAMIZI DHIDI YA SEYYIDNA AHMAD[AS] KUWA KWAKE IBN MARYAM

بسم الله الرحمٰن الرحيم

Vivyo hivyo, Masihi

7. Katika wayahudi walimkataa Issa na wakamkadhibisha na wakataka kumuua na wakampeleka mbele ya mahakimu, na hivyo ndivyo walifanya baadhi ya maulamaa wa kiislam walimkufurisha na wakamkadhibisha na wakampeleka kwa mahakimu katika mahakama ya kiserikali na walifanya kila aina ya juhudi kwaajili ya kumuuwa na kwasababu yeye alikuwa ni Mtume mkweli aliye tumwa na Mwenyezi Mungu basi hila hizo za wapinzani hazikutimia, sawa na ahadi yake mwenyewe " Atakulinda mbele yake hata kama watu hawatakurinda". Na nikweli kwamba Mtume saw alikuwa fasaha kuliko watu wengine, basi hivyo alivyosema kuhusiana na Masihi aliyeahidiwa kufika kwake kwa maana ya kimethali:
"Mtakuaje atakapoteremka Isa Ibn Maryam kati yenu na Imam wenu miongoni mwenu"
" Mtakuwaje atakapoteremka ibn Maryam kati yenu basi na akawaongoza" .
Mtume[saw] anaashiria ya kuwa yeye atakuwa mtu miongoni mwa watu wa Muhammad[saw].

Hivyo ndivyo ilivyo habari ya ujaji wa mara ya pili tunaye mwamini. Ilikuwa karibu miaka miamoja na kitu hivi iliyopita ya kuumbwa mja mnyenyekevu wa Mwenyezi Mungu, jina lake Mirza Ghulam Ahmad wa Qadiani alipashwa habari na Mwenyezi Mungu ya kuwa yesu mnazareti na mwana wa Maryam ambaye ujaji wake wa mara ya pili unangojewa na waislam na wakristo kwa usawa, alikuwa nabii maalumu wa Mungu aliyekwisha kufa tayari, kama walivyokufa manabii wengine wa Mungu. Hazrat Mirza Ghulam ahmad a.s alitangaza kuwa yesu hayuko hai kimwili wala hakupaa mbinguni akisubiri huko kurejea tena kuitembelea ardhi, alikwisha kufa kama manabii wengine wa Mwenyezi Mungu wala hakuwa zaidi ya manabii.

Ujaji wa pili wa yesu kristo unaoaminiwa na wakristo na waislam kwa pamoja ulimaanisha ni kutokea kiroho sio kidhahiri. Ndivyo alivyoambiwa Hazrat Mirza Ahmad a.s na Mungu. Na akapashwa habari pia ya kwamba Mungu amemtuma yeye ili kutimiza bishara hiyo ya ujaji wa yesu kristo kwa mara ya pili.

ATAKAYE MKATAA MASIHI NA IMAM MAHD NI KAFIRI

Mwenyezi Mungu anasema ndani ya kuran tukufu kwamba:

أَفَمَن كَانَ عَلَى بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّهِ وَيَتْلُوهُ شَاهِدٌ مِّنْهُ وَمِن قَبْلِهِ كِتَابُ مُوسَى إِمَامًا وَرَحْمَةً أُوْلَـئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ
وَمَن يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الأَحْزَابِ فَالنَّارُ مَوْعِدُهُ فَلاَ تَكُ فِي مِرْيَةٍ مِّنْهُ إِنَّهُ الْحَقُّ مِن رَّبِّكَ وَلَـكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لاَ يُؤْمِنُونَ

'' Basi je,{anaweza kuwa muongo} yule ambae anadalili iliyo wazi kutoka kwa Mola wake na shahidi mmoja kutoka kwake atamfuata, na kabla yake kulikuwa na kitabu cha Musa kilichokuwa kiongozi na rehma? Hao wanamwamini yeye, na atakaye mkataa katika makundi mbalimbali, moto ndio utakuwa mahari pake pa miadi basi usiwe na shaka kuhusu jambo hili. Hakika hii ni haki itokayo kwa mola wako, lakini watu wengi hawaamini" {sura 11:18}

◎ Mtu aliye na dalili waziwazi, yaani Mtume saw amabaye ukweli wake na ukweli wa mafundisho aliyoleta umethibitika. Shahidi mmoja atokae kwake atamfuata. Shahidi hutakiwa kwaajili ya kuhakikisha jambo. Wakati mafundisho ya kiislam yamefanyiwa shaka hasa ni baada ya miaka 1350. Kuna baadhi ya waislam wenyewe wanaofikiri mafundisho ya Qurani, hasa ya sala tano za kila siku kukata mikono ya wezi, kuowa wake zaidi ya mmoja , wanawake kufunika nyuso barabarani na kuto changanyika ovyo na wanaume wasio kuwa jamaa zao, riba n.k kwamba yanahitaji kubadilishwa.

◎ Kunawatu wanaofikiria kuwa sheria ya kiislam imetanguka na wanataka kuleta sharia mpya mahala pake. Kuna hao wapinzani wa ulaya na Amerika wanao dadisi usahihi wa baadhi ya mambo ya historia yaliyotajwa na Qurani, na pia wakilaumu kuwa mafunzo mengine ya Qur-an si mazuri kufuata. Mambo kama haya hayakupata kutokea kabla ya zama hizi, na bila shaka kabla yake hapakuwa na haja ya shahidi. Shahidi huyo aliyefika ni mjumbe wa Allah yaani Seydna ahmad a.s yaani Masihi na Mahdi aliyeahidiwa ambaye alianzisha huu mwendeleo huu wa Uislam uitwao Ahmadiyya wakati ambao mafundisho ya Islam yalipo kataliwa na watu wazi wazi na kabla yake kulikuwa na kitabu cha Musa a.s ambacho kina bishara nyingi za kufika mtume s.a.w. Hizi ndizo dalili 3 za kuhakikisha ukweli wa Mtume saw na ukweli wa dini ya kiislam.

◎ Kiongozi na rehma, kwasababu kimewaongoza watu kwenye ukweli wa dini ya kiislam na kime wafanyia rahisi kukubali ukweli wa dini ya kiislam kwa kueleza bishara zinazoonyesha ukweli wa mtume[saw].
◎ Kwasababu kimeweka mizani ya kuhakikisha ukweli wa Nabii yeyote Kwakuwezesha watu kulinganisha mafundisho ya vitabu viwili. Na kwakusaidia kufafanua kanuni za kisheria. Nimuhimu kuainisha kijina hao kinamrejea nani? Watu wawili pekee waliotajwa kwenywe aya hii ni Mtume s.a.w na shahidi kutoka kwa Allah. Ama kumuhusu Musa si yeye bali ni kitabu chake ndicho chenye kurejewa na vitabu haviamini. Tunabakiwa na chaguo moja tu kwamba kundi la watu ndilo linalo rejelewa katika aya hii. Kijina hiki cha mrejerelea siye tu mtume mwenyewe pia mtu aliyechini yake ambaye ni shahidi na baadhi ya watu wengine. Aya hiyo ni lazima ieleweke katika maana hiyo hiyo kwamba siye Mtume tu na shahidi wake ndiyo wanao uamini ukweli wa Mtume saw na kuutolea ushuhuda bali idadi kubwa ya wafuasi wao nao pia wanafanya vivyo hivyo.

Sasa kwa kutokana na aya hii maswali mengi huzuka vichwani mwa watu je ninani huyo shahidi atakae mfuata na je, atakayemkataa shahidi huyo ni kafiri?
Swali linazuka : Je, mtu anayemkana Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s (Masihi aliyeahidiwa) anahesabiwa kuwa kafiri?

Pingamizi: Inadaiwa kwamba Hazrat Mirza Ghulam Ahmad alitoa hukumu ya ukafiri dhidi ya Waislamu wote wanaomkana.
Pingamizi hili linatokana na maandiko yake yafuatayo:

"Mwenyezi Mungu amefunua kwangu kwamba kila mtu ambaye ujumbe wangu umemfikia na hajanikubali, si Muislamu."* (Tadhkirah, uk. 519)

Jibu la swali hilo ni kama ifuatavyo Kauli iliyotolewa ni sehemu ya barua ambayo Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s alimwandikia Abdul Hakim. Swali hili lilijitokeza wakati wa uhai wa Masihi aliyeahidiwa, na alijibu kwa undani katika kitabu chake "Haqiqatul Wahyi". Kabla ya kuelezea swali na jibu la kina la Hazrat Ahmad, ufafanuzi wa jumla unahitajika.

Kwa hakika, madhehebu mengi makubwa ndani ya Umma wa Kiislamu, ingawa yanakubali kwamba wote wanaokiri kalima (tamko la imani) ni Waislamu na wanaamini ukweli wa Mtume Muhammad[saw], bado wanatoa hukumu za ukafiri dhidi ya wengine kutokana na tofauti za kiitikadi. Hata hivyo, wakati Waislamu wa Ahmadiyya wanapotoa hukumu ya ukafiri, ni kwa sababu Waislamu wengine huwafungulia wao hukumu ya ukafiri kutokana na kumkataa kwao Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Kulingana na hadithi ya Mtume[saw], Muislamu anapomwita Muislamu mwingine kafiri, tuhuma hiyo inarudi kwa mtuhumu mwenyewe.
Mtume Muhammad[saw] alisema:

"Muislamu yeyote anayemwita Muislamu mwenzake kafiri, kama tuhuma hiyo si kweli, inarudi kwake mwenyewe."
(Sunan Abi Dawood, Kitab al-Sunnah)

Kwa hivyo, ni mantiki na kimaandiko kwamba Waislamu wa Ahmadiyya wanapaswa kumwona kafiri yule anayemkana Imamu wao, aliyeteuliwa na Mungu. Hii siyo shutuma ya uongo, bali hali ambayo wengine wanaona fahari kwao kwa kumtangaza Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s kuwa kafiri. Ikiwa wanajivunia hili, kulingana na hadithi, hukumu yao ya ukafiri inarudi kwao wenyewe, na hawapaswi kujisikia vibaya kwa hilo.

Swali na Jibu la Hazrat Ahmad a.s: Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s ameandika mara nyingi kwamba kumwita kafiri mtu anayesoma kalima au anaye elekea kibla si sahihi. Hii inaonyesha wazi kwamba, mbali na wale wanaomkana na hivyo kuwa makafiri, kumkataa yeye pekee hakumfanyi mtu kuwa kafiri. Hata hivyo, ulimwandikia Abdul Hakim Khan ukisema kwamba yeyote ambaye amesikia ujumbe wako na hajakukubali si Muislamu. Kauli hii inaonekana kupingana na maandiko yako ya awali, kama vile {Tiryakul Qulub}, ambapo ulisema kuwa kukukataa hakumfanyi mtu kuwa kafiri.

Itaendelea toleo Lijalo

Bustani ya Washairi

POKEA ZETU DUAU

Jina lako ni muhimu, Mola Mwenye asmau.
Naitumia nudhumu, kukuletea duau.
Na tumwa wetu Hashimu, nimtakie shufau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Ya Rahamani Rahimu, Mola usiye nahau.
Twaomba kwako naimu, na baraka anuau.
Utuwezeshe nidhamu, tuishike ahayau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Ya Ilahi ya Dawamu, Mola Muumba samau.
Tulio kundini humu, utupe mema walau.
Utuwezeshe kudumu, tukitii khulafau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Ewe Hayyul Qayyumu, usiye na abnau.
Utuzidishie ghamu, ibada tusisahau.
Utufanye maasumu, maasi tuyasahau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Ya Bariu ya Karimu, Mola mwingi wa Shufau.
Waja wako mahamumu, twaomba yako liqau.
Tufanye tuwaheshimu, hata wanotudharau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea

Laaliyyu Laadhimu, Mkuu wa kubarau.
Tupe afiya timamu, Rehema yako dawau.
tuepushe na magumu, yanayoleta fazau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Ni Alimu na Hakimu, mwenye fani anuau.
Tuzidishie elimu, nasi tuwe fukahau.
Kiroho tupe makamu, daraja uturufau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Ndiwe Mpaji muhimu, Razaku uso khatwau.
Turuzuku vya utamu, tende hadi zambarau.
Shibisha yetu kaumu, kwa chapati na pilau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Ndiwe Azizu Halimu, utukinge na jinau.
Tupe mahaba adhimu, tuwe watu ruhamau.
Na mbele ya mahasimu, utufanye ashudau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Muhammadi Muungamu, Bwana wa anbiyau.
Mpe sala na salamu, kwa ulufu si miyau.
Ili siku ya kiyama, atutakie shifau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Masihi wake Ghulamu, Khatamu wa khulafau,
Mzididhie kaumu, ya wema na hukamau.
Ashindishe Isilamu, wahemewe sufahau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Khalifa wetu imamu, Masruru Mirzau.
Mpe kinga maalumu, dhidi yao manyang'au.
Umshushie farumu, ya neema za matau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Inusuru tanzimu, ya wale watu abau.
Ansaru wa hirimu, wazee washika dau.
Wape maisha matamu, marefu yenye nufau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Pia ile ya khudamu, baro baro ashijau.
Komaza zao jusumu, wasiwe vimbau mbau.
Ili wakaze gidamu, mbele ya majuhalau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Wanawake wahashamu, wale lajina imau.
wajaze utaalamu, usio na au au
Wasichoke kukirimu, wanyonge na dhuafau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Hapa natua kalamu, nipumzike walau.
Nimetimiza jukumu, la muombaji khashau.
Mola wetu Mkarimu, ndiwe Mujibu duau.
Pokea zetu duau, Rabi twakuelekea.

Abu Talha, Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi)
99.3 Radio Ahmadiyya Mtwara.
kungwi504@gmail.com

Ndoa zilizo dumu

Ndoa zilizo dumu, ni zile za wajinga
Kwenye nyakati ngumu, wakajifanya wajinga
Juaji kwao Sumu, elekezo so Pinga
Ndoa zilizodumu, nizile za wajinga

Ndoa zilizodumu, nizile za wanyonge
Ubishini so dumu, wakakubali unyonge
Kikosa watadumu, tobani wasisonge
Ndoa zilizo dumu, nizile za wanyonge

Ndoa zilizodumu, zawale waloshindwa
Wakashika nidhamu, shetani wakalindwa
Walojipa jukumu, toroka waloshindwa
Ndoa zilizodumu, zawale waloshindwa

Ndoa zilizodumu,ni zile za washamba
Starani walodumu, wasopenda kujigamba
Anasa sohudumu,wazichungao nyumba
Ndoa zilizodumu, ni zile za washamba

Ndoa zilizodumu, zile za walemavu
Bubu wasousemu, kutosema momivu
Viziwi vipofumu, walemavu maovu
Ndoa zilizodumu, zile za walemavu

Iliyako idumu, kiburi kizuwiye
Wemani we udumu, apanda jishushiye
Mwenzo mpe muhimu, dharau sifanyie
Ndoa zilizodumu, zile za wema

Nasimamisha kalamu, wajinga meelewa
Ndoa zetu zidumu, kiburi kuondowa
Heshima na nidhamu, makosa samehewa
Ndoa zetu tadumu, wajinga meelewa

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

KUNGURU

Ogopa aloshukuru, kwa yote uliyotenda
Wingi kakarakukuru, kumuachia kidonda
Usimanye uko huru, hutoonja chungu tunda
Majuto huja mwishoni, usicheze na kunguru.

Na Mahmood Hamsin Mubiru –Wamamba Kiwalani - Dar es salaam.

MAMA UMETUPONYOKA

Astahabu salama, kote ninakosikika.
Naimba nikilalama, msiba umenifika.
Ninamlilia mama, Bi Marunda kanitoka.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Ingawaje walisema, manju waliotukuka.
Huna baba huna mama, uwe na Mola Rabuka.
Wa ila kifo cha mama, punde moyo hupasuka.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Mama yetu bi Salima, mpwa wa Kaimba Nyaka.
Ulikuwa mja mwema, muumini uso shaka.
Amekuita Karima, witowe ukaitika.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Akurehemu Karima, kwa pepo ilotanuka.
Mama usiye hasama, sasa umetuondoka.
Ukiwani tumezama, machozi yatiririka.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Ulihimili zahama, kulea wa kila rika.
Ukawaenzi kwa wema, yatima walodhikika.
Ulizibeba nakama, bila ya kukirihika.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Ni mwanamke wa chuma, dhiki hukuzisituka.
Hofu ilioposakama, kamwe hukutetemeka.
Na katu haukunema, ulipogusa fanaka.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Ulikuwa maamuma, ila hukughilibika.
Kidete ulisimama, kwa hoja za uhakika.
Ulijaliwa hekima, na sudi ilopevuka.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Kwa sala tano daima, hukuwahi pepesuka.
Usiku ulisimama, hata ulipozeeka.
Kumsabihi Rahima, mama hukughafilika.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Hukusita kujinyima, umtolee Rabuka.
Kwa mazao ulolima, ya mizizi na nafaka.
Ulitoa takirima, wengi tukafaidika.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.


Ni mwalimu wa heshima, ulofundisha khuluka.
Masugu waloparama, mbele yako walinyoka.
Leo ni watu wazima, tena wa kuheeshimika.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

innalillahi twasema, kwa Mungu twajipeleka
Tunaomba Allahumma, peponi atakuweka.
Na sisi tulio nyuma, subira tuweze shika.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Ukumbi ninauhama, vina vimenipunguka.
Nawahi Darisalama, nishiriki kumzika
Haiba yake daima, wana tutaikumbuka.
Mama umetuponyoka, akurehemu Manani.

Abu Talha, Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi)
99.3 Radio Ahmadiyya Mtwara.

Unganisha Nukta kupata Mchoro



MANENO YA SEYDNA AHMAD[as] JUU YA QUR AN TUKUFU

Aliyeahidiwa[as] Kurani Tukufu ndicho kitabu chenye fahari kuu kiasi hiki kwamba hapana kitabu kingine kinachoweza kuipita katika fahari yake. Ndicho Al-Hakam, kikiwa kitabu ambacho uamuzi wake ndio wa mwisho; ndicho Muhaiman, yaani:

Ni muhtasari mzima wa kila mwongozo. Ndani yake yapatikana kila hoja mtu awezayo kuhitaji.

Ni kitabu hiki ambacho kimeitimua kwa ushindi nguvu ya maadui. Kitabu kinachozungumzia kila kitu kwa undani na kinazo habari za yale yaliyokuwepo na yale yatakayo kuwepo.

Batili haiwezi kukishambulia toka mbele wala nyuma. Ndicho nuru halisi ya Mungu Mweza.

(Roohani Khazain Jal. 16, Uk. 103: Khutba Ilhamiya Uk. 103).

JINSI YA KUTENGENEZA KEKI

VIPIMO VYA CAKE
KEKI YA ROBO

Unga kikombe 1
sukari nusu kikombe
siagi nusu kikombe
bakingpoda kijiko kidogo 1
mayai 3-5
tin nch 6/7



KEKI YA NUSU
Unga vikombe 2
sukari kikombe 1
siagi kikombe 1
mayai 4-8
bakingpoda kijiko cha chakula 1
TIN nch 8

KEKI YA KILO
Unga vikombe 4
sukari vikombe 2
siagi vikombe 2
mayai 8-16
bakingpoda vijiko 2 vyachakula
TIN nch 10

TUMIA KIKOMBE KIKUBWA KAMA UNATUMIA MEASURING CUPS, KAMA HUNA TUMIA KIKOPO CHA BLUEBAND CHA ROBO KILICHOANDIKWA 250g

KIKOMBE 1=ROBO=250g
VIKOMBE 2=NUSU=500g
VIKOMBE 4=KILO=1000g

HEKIMA YA DHABIHU

Asemavyo Masihi aliyeahidiwa[as]
(Gazeti la Badr, 14 Feb 1907)

Asemavyo Masihi aliyeahidiwa[as] Anasema Hazrat Masihi Aliyeahidiwa[as]: "Allah Ameeleza mifano katika sheria ya kiislamu kwa ajili ya maamrisho muhimu. Kwa mfano, mwanadamu ameamrishwa ajitolee katika njia ya Allah kwa nguvu zake zote na mwili wake wote. Basi dhabihu za kidhahiri zimefanywa kuwa mfano kwa hali hiyo. Lakini shabaha hasa ndiyo dhabihu anayoeleza Allah

لن ينال الله لحومها ولا دماؤها ولكن يناله التقوى منكم

yaani nyama za dhabihu zenu hazimfikii Mungu wala damu yao lakini unamfikia utawa wenu- yaani mcheni mpaka mkajifie katika njia yake na jinsi mnavyochinja dhabihu kwa mikono yenu kadhalika mjitolee katika njia yake" *(Chashma'e Ma'arifat, Uk. 99)*

UTAKASO WA NYOYO
"Utakaso wa nyoyo ndio dhabihu ya kweli, nyama na damu sio dhabihu ya kweli. Watu wa kawaida huchinja wanyama lakini watu maalumu huchinja nyoyo zao. Allah hakuzuia dhabihu hizi pia ili ijulikane kuwa dhabihu hizo pia zinamhusu mtu." *(Barahin-i- Ahmadiyya, juz. 5)*

UBORA WA MAFUNDISHO YA UISLAMU
"Mimi nadhamba dhabihu hizi katika sheria yetu ng'avu hazihesabiki, na zinazishinda zile dhabihu za nyimati za hapo kabla. Wingi wa dhabihu umefikia hadi kwamba uso wa ardhi umefunikwa na damu, hata kwamba kama damu zao zote zingekusanywa pamoja na kutaka kuzitiririsha, kwa
yakini mifereji ingeanza kupita kwa hizo, na mito kutiririka, na maeneo yaliyo katika nyanda za chini na mabonde makubwa yangefurika na damu. Na kitendo hiki chahesabiwa katika dini yetu katika yale mambo yanayomsogeza mtu karibu na Allah." *(Hotuba iliyofunguliwa, UK. 41)*

NANI ATOE DHABIHU?
Mtu mmoja alimwandikia barua Masihi Aliyeahidiwa[as] na kumuuliza kwamba mimi nilichangia kiasi cha pesa kidogo kwa ajili ya kutoa dhabihu ya pamoja lakini watu wengine waliniondoa kwenye wachangiaji kwa sababu mimi nilikuwa mwahamadiyya. Je, yafaa kwangu kutoa dhabihu nikitoa kiasi hiki cha pesa kwa ajili ya mchango wa sadaka hapo Qadian?

Akasema:
"Dhabihu hutolewa kwa kuchinja mnyama na si kwa kutoa pesa katika mfuko wa mchango wa sadaka. Ikiwa kiasi kile kinatosha basi toa dhabihu ya mbuzi mmoja, na kama hakitoshi na huna uwezo wa kuongeza basi si faradhi kwako kutoa dhabihu."

K U S H I R I K I A N A KATIKAKUTOA DHABIHU
Mtu mmoja aliuliza swali kwamba je, inasihi kuchinja mnyama kama vile ng'ombe kwa kuchangia pesa kidogo kidogo pamoja na wasiokuwa waahmadiyya?

Akasema:
"kuna haja gani ya kushirikiana na wasiokuwa waahmadiyya. kama kutoa dhabihu ni faradhi kwako basi unaweza kumchinja mbuzi na kama huna uwezo huu basi si lazima kwako kutoa dhabihu. Hawa wasio kuwa wahmadiyya wanakuita kafiri hawapendi kushirikiana na wewe basi kwa nini unataka kushirikiana nao? Mtegemee Allah." *(Gazeti la Badr, 14 Feb 1907)*

MNYAMA WA AINA GANI HUCHINJWA?
Mtu mmoja alimuuliza Masihi Aliyeahidiwa[as] kwamba kama hatupati mnyama ambaye anakidhi vigezo vilivyoelezwa katika Hadithi je, inasihi kumchinja mnyama mdogo?

Akasema: Inafaa wakati kuna ulazima lakini siku hizi hakuna ulazima kama huu. Mtu anaweza kutafuta mapema kwani siku zinatosha, hivyo hairuhusiwi kutafuta njia au kuonesha uvivu bila sababu." *(Gazeti la Badr, 23 Jan 1908)*

KUFUNGA SAUMU SIKU YA IDUL ADH'HAA
Khalifatul masihi wa pili[ra] akieleza kuhusiana na kufunga saumu siku ya idul-adh'haa na kufungua kwa kutumia nyama ya dhabihu.

Anasema:
"Maulawii Muhammad Ibrahim wa Bakaa Pur aliniandikia kwamba itangazwe kuwa saumu inayofungwa siku ya Eid si sunna ya Mtume[saw]. Hii ilikuwa ni kawaida ya Mtume[saw] kwamba alipokuwa na afya nzuri alianza kula kwa kutumia nyama ya dhabihu. hata hivyo hii si saumu kama vile mtu asipoifunga atakuwa amekosea.

Hii si saumu ya faradhi ni ya nafali na inasisitizwa kwamba anayeweza afunge kwa muda kidogo lakini ambaye ni mgonjwa mwingine asipoifunga si faradhi kwake wala hatapata dhambi. Pamoja na hayo ikumbukwe kwamba si sahihi kusema kuwa saumu hii haipo kabisa katika sunna kama alivyoandika Maulawii Bakaa Puri.

Mimi niliwahi kumuona Masihi Aliyeahidiwa[as] akitekeleza fundisho hili alipokuwa na afya nzuri. Pia imezoeleka sana katika waislamu na haiko hivi bila sababu ni nafali inayosisitizwa na Mtume[saw] alikuwa akiendelea kutekeleza jambo hili na atakayefanya hivi atapata thawabu lakini asipoweza hana dhambi."

MATUKIO KATIKA PICHA













Mtumishi Mnyenyekevu wa Allah | Simiyu Inayopaa na Kunguruma

Na Dkt. Haroun Salum Mgeleka



Tangu tulipohamia Mkoa wa Simiyu katika majira ya baridi ya mwaka 2020, ratiba yetu ya asubuhi ilibadilika.

Asubuhi zetu hazianzi tena na kikombe cha kahawa, bali na mfululizo wa ujumbe wa WhatsApp kutoka kwa Sheikh Ali Dino Tahir.

Kwa haiba; Sheikh Dino ni mrefu, mwembamba na mnyenyekevu. Anayetunza ndevu zake na Daima kichwani huvaa kofia, mtumishi wa Mungu aliye na uthabiti usioyumba — Sheikh Ali Dino ameweka kiwango cha juu sana, akiwa mfano wa kuigwa kwa ma Sheikh wote.

Ingawa si maarufu miongoni mwa wenzake akitawaliwa na haiba ya ukimya na maneno machache mdomoni— Sheikh huyu amehuisha mikoa ya Simiyu na Mara kwa viwango vipya vya utumishi kwa Allah. Ameweka Mzani juu sana katika huduma.

Kwa makusudi, amewageuza waliojiunga na Jamaat hivi karibuni kuwa Waislamu wa Ahmadiyya waliojaa imani na msimamo thabiti. Amejenga msingi usiotikiswa kwa vizazi vijavyo!

Kwa miaka miwili na nusu iliyopita, Maulana Ali Dino ameendesha makambi ya Tarbiyyat kila mwisho wa wiki, yanayovutia watoto na vijana wanaohifadhi maswali na majibu kutokana na mafunzo maalum ya maswali kwa mamia kuhusu sira ya Mtume Muhammad[saw] na maswali mengine ya Dini tukufu ya Kiislam yasiopungua 2000

Anaandaa makambi matatu kila mwezi, kila moja likiwa na washiriki kati ya 50 hadi 70. Ubunifu huu umekuwa kiini muhimu kwa Tarbiyyat.

Akiwaongoza zaidi ya Jamaat 45 na Maalim 20 katika mikoa ya Simiyu na Mara, uongozi thabiti wa Maulana umewezesha kuanzishwa kwa madarasa ya kawaida kwa matawi yote anayoyasimamia.

Siyo tu kwamba Maulana Sheikh Ali Dino anaendesha makambi ya Tarbiyyat, bali pia ameendeleza jitihada zake kupitia majukwaa ya kidijitali. Kituo chake cha YouTube, 'Upendo Kwa Wote', kimepanua zaidi ujumbe wake.

Chaneli hii ndo chaneli kinara kuliko YouTube zote za Jamaat Tanzania, ikiwa na zaidi ya wafuatiliaji 8,300 na video zaidi ya 5,400. imeendelea kuwa chanzo cha msukumo na chemchemi ya maarifa.

Kupitia YouTube, utaona shamrashamra na hewa safi ya shauku miongoni mwa watoto katika makambi kila mwisho wa wiki. Pia, utaona watoto na vijana wengi wakisoma Qur'an, Tafsiri ya Quran neno kwa neno, mashairi, na kujibu maswali kuhusu mada mbalimbali — ishara ya kukua kwa fikra zao.

Alizaliwa na kulelewa Kusini mwa Asia — katika mazingira tofauti kabisa. Hata hivyo, ameweza kuishi na kuelewana vizuri katika jamii yenye tamaduni, lugha na rangi mbalimbali. Ameweza kuwa sehemu ya jamii hii kwa namna ya kipekee.

Maulana Ali Dino, anayeishi kwa unyenyekevu na ambaye hana tamaa ya mali, ni mcha Mungu ambaye amejenga uhusiano wa dhati na jamii ya Wasukuma na Wakurya. Uhusiano huu umeimarika kwa muda, kiasi kwamba sasa jamii haimheshimu tu Sheikh Ali Dino, bali pia wanampenda na kumshukuru kwa dhati.

Katika kambi ya karibuni ya Tarbiyyat, watoto walimkaribisha kwa zawadi walizotengeneza kwa mikono yao — ishara ya upendo na uaminifu uliomea kati yao.

Maulana amejiwekea dhamira ya dhati ya kuhakikisha elimu na mafunzo ya Tarbiyyat yanarithiwa na vizazi vijavyo. Hivi karibuni, Jamaat Ahmadiyya ilimpatia gari kwa ajili ya huduma za kidini Simiyu.

Analitumia kusafirisha watoto kwenda makambini na kwa shughuli nyingine muhimu.

Makambi haya yanaendeshwa kwa michango midogo kutoka kwa wenyeji — nafaka, unga, mchele, maharage, na sarafu chache — pamoja na msaada kutoka Makao kuu, Yameonyesha kuwa na matokeo makubwa, ni ya vitendo na ya gharama nafuu. Somo ambalo linaweza kuigwa nchi nzima.

Katika miaka kumi ya huduma yake hapa Tanzania, Sheikh Ali Dino tayari ameacha alama kubwa — kutoka Redio ya Mtwara hadi mioyo ya mamia ya Atfal, Nasrat na Khuddam wa Nangale, Kisesa, Itilima, Mitobo, Bariadi, Mwaukoli, Muhunze, Mwabuma, Tarime na maeneo mengine mengi!

Hisia na uhusiano huo vitaendelea kudumu kwa miaka mingi ijayo.

Katika maeneo ambayo awali yalikuwa kimya, sauti ya UPENDO KWA WOTE sasa ni chemchemi ya harakati za imani, elimu, na ustawi. Akiwaacha watu na urithi wa kudumu kwa vizazi vijavyo.

Maulana Maulvi Sheikh Ali Dino haongozi tu makambi ya Tarbiyyat, bali pia amepanua wigo wa huduma zake kupitia majukwaa ya kidijitali. Kituo chake cha YouTube, 'Upendo Kwa Wote', kimeongeza maradufu athari ya ujumbe wa Jumuiyya ya Waislamu Waahmadiyya

Sheikh ALI Dino alianzisha kituo hiki cha YouTube akiwa Mkoani Mtwara ,mwanzoni kilikuwa kwa ajili ya Mahubiri na Historia ya Wanajumuiyya kisha ameunganisha Video za Malezi

Katika maeneo ambayo awali yalikuwa kimya, sauti ya Upendo Kwa Wote sasa imechochea harakati za kudumu za imani, elimu na ustawi — akiacha urithi wenye uzito kwa vizazi vijavyo.

Inshallah, Jina la Sheikh Ali Dino, litatajwa pamoja na Magwiji Kama Maulana sheikh Mubarak Ahmad, Maulana Hafiz Suleiman, Sheikh Muhammad Munawar, Maulana Jamil Rafiq, Maualana Kaluta Abeid, Sheikh Inayatullah Chaundry, Maualana Jalaludin Qamar. Akina Sheikh Swaleh Mbaruk Kapilima, Sheikh Maqbul Zabih na Maualana Bashir Akhtar — Akiingia katika Ulingo wa ma Maulaama



Maulana Sheikh Ali Dino Tahir (Sahib)

MAISHA YA MOHAMED IQBAL DAR (1944 – 2025)

Kutoka uk. 12

ubaga katika kitabu; "Nani Aliyebuni Jina Tanzania".

Mwaka 1965 alihamia Uingereza ambako toka mwaka 1966 hadi 1969 alikuwa katika Chuo cha Chambers London alikopata Diploma katika uhandisi wa Radio na Runinga. 1972 alikuwa Chuo cha British Institute of Engineering alikopata Diploma katika ufundi na utengenezaji wa Runinga. Baada ya masomo yake aliamua kujiajiri na alifanya kazi ya kujiajiri kwa ufanisi mkubwa.

Siri yake kubwa ya mafanikio ilikuwa ni ukweli na uaminifu. Kabla hatujaendelea kuyatazama maisha ya Iqbal Dar kwa undani ninadhani itakuwa ni jambo la busara kuyatazama pia kwa undani maisha ya Dr. Tufail Ahmad Dar, kwani ni Dhahiri shahiri ya kwamba Mohamed Iqbal Dar alimpenda sana baba yake na alimuathiri sana katika maisha yake. Katika barua yake aliyoniandikia mwezi Agosti, 2024 aliniambia kuwa aliandika kitabu juu ya baba yake na kukipa anuani "Mohamed Iqbal Dar a Life in words and a legacy of Dar Family Tree". Mohammed Iqbal alikuwa Mshairi mzuri wa lugha ya Kiingereza na aliwahi kunitumia shairi juu ya baba yake katika lugha ya Kiingereza. Nalitafsiri katika lugha isiyo rasmi ya kishairi ili kudhihirisha hoja ninayojenga ya kuwa Mohammad Iqbal Dar alimpenda na kumheshimu baba yake.

Daktari mahiri, aliyejaa maziwa ya huruma kwa wote,
Na daima akiwa na matumaini na kesho, Mtu mnyoofu ambaye hakudhihirisha huzuni,
Aliyeamini kwa dhati Allah na sifa zake lakini yote haya, ulipotokea mgogoro na watu wake wa karibu. Kila kitu alikiweka pembeni, na kukimbilia kwa Mola wake.
Daima alitoa kipaumbele kwa mafundisho ya Islam
Bwana mwenye Imani bila kujali chochote kile
Kaonesha Daktari,
Mfano ulo mzuri,
Hadi akamuathiri,
Kijanae shabaruni.

ATHARI ZA BABA KWA MWANAE

Watoto huathirika,
Na vichwa vyao hushika,
Yale yanayotendeka,
Nao wazazi nyumbani.

Hivyo tunao wajibu,
Kufanya yalo twaibu,
Yasiyoleta aibu,
Kuwaweka hasarani.

Kwa kiwango kikubwa Mohammed Iqbal Dar alifanikiwa kukanyaga nyayo alipokanyaga baba yake. Ndiyo maana Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ametushauri kuwapa watoto majina mazuri. Kuna jina gani linaloweza kuwa bora na tamu kuliko Muhamamad? Anayestahili kusifiwa. Na jina la pili la kijana huyo Iqbal ambalo lina maana pana na baadhi ya sifa za jina hilo ni; Ni bahati nzuri, kufika kwenye kilele cha ustawi, furaha, neema na Baraka.

Dr. Tufail Ahmad Dar alikuwa na bidii katika masomo yake na hakuna kitu alicho kienzi kama elimu. Daima ile aya ya; "Rabbi Zindii 'ilmaa" ilikuwa moyoni mwake. Nyumbani kwake alikuwa na Maktaba iliyosheheni vitabu na majarida yaliyohusu Utabibu ambayo aliyaagiza kwa gharama kubwa na akawa anayosoma. Kitu cha kwanza kilichowavutia watu waliotembelea nyumbani ni vitabu vilivyokuwa katika chumba cha mazungumzo.

Mwenendo huo wa kuwa rafiki wa vitabu aliurithi Mohammed Iqbal Dar, alikuwa msomaji mzuri wa vitabu vya dini, falsafa, fasihi na historia. Lakini ikumbukwe utamaduni huo ulianza toka yupo shuleni. Ni kwa masikitiko makubwa kwamba hivi sasa utamaduni huo wa kuwa na Maktaba na kuwahimiza vijana wasome si kwa ajili ya mitihani tu haupo. Lakini ni mwenendo huo mzuri wa kusoma vitabu uliomsaidia Mohammed Iqbal Dar kujenga mapenzi yake na vitabu. Lakini sifa nyingine ni kwamba ni mwenendo huo huo wa kupenda kusoma uliofanya shule ya Mzumbe kumchagua kuwa Msimamizi wa Maktaba ya shule. Ni mwenendo huo huo wa kupenda kusoma uliomsukuma kwenda kwenye Maktaba ya shule alikosoma gazeti la 'The Standard' ambalo alisoma tangazo la shindano la kuhsu jina jipya kwa ajili ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kwa masikitiko makubwa turudie kusema utamaduni wa kujisomea umetoweka kabisa nchini. Sasa hivi mwanafunzi hasomi kutokana na raha ya kusoma, bali kinachomsukuma kusoma ni kufanya mitihani. Mitihani ikiisha, vitabu vinatelekezwa. Utamaduni huo wa kupenda kusoma, unatakiwa ufufuliwe, kwani Taifa haliwezi kuendelea bila kujenga utamaduni wa kusoma. Wakati nikiwa Katibu wa Elimu Taifa wa Jamaat, palikuwa na uhaba wa vitabu mashuleni, Mohammed Iqbal Dar alisaidia sana kununua vitabu kwa ajili ya wanafunzi na kuwanunulia sare za shule na kuwalipia karo.

Kwa kiwango kikubwa, Mohammed Iqbal Dar ana mchango mkubwa katika kuandika historia ya Ahmadiyya katika Tanzania. Yeye amekuwa kichocheo kikubwa. Historia ya Ahmadiyya Tanzania imetokana na msaada wake mkubwa wa hali na mali. Hivi leo ingawaje si sana lakini angalau yameandikwa kwa uchache kuhusu historia ya Ahmadiyya Tanzania. Hii ni kazi kubwa na wapo waliosaidia sana katika kuhakikisha historia ya Ahmadiyya na kuhifadhiwa. Khalifatul Masih –V (atba), Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) aligharamia kuchapisha kitabu; *"Ahmadiyya na Ukombozi wa Tanzania"*. Mohammed Iqbal Dar alitoa mchango katika uchapishaji wa kitabu cha; *"Historia ya Ahmadiyya Tanzania"*, *"Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya"* na *"Nani aliyebuni jina Tanzania"*. Pia aligharamia uchapishaji wa *"Almasi ya Afrika"* na *"Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri"*.

.Wapo baadhi ya watu wakishahama mahala hutupa jongoo na mti wake! Hawaulizi chochote kuhusu mahali hapo. Lakini haikuwa hivyo kwa Dr. Tufail Ahmad Dar, yeye aliendelea kuwa na uhusiano katika nchi alikoishi kwa takribani miaka 40. Aliendelea kuandikiana na Masheikh na wananchi ili kufahamu yaliyokuwa yanaendelea nchini. Na katika barua hizo kwa Mashiekh na marafiki zake, alisema hajaisahau Tanzania na daima anaiombea. Mwaka 1965 alitoka Tanzania na kwenda kuishi Faislabad –Pakistan. Umbali haukumtenganisha na Tanzania kwa kupitia barua na magazeti aliendelea kufahamu yaliyokuwa yanaendelea nchini. Mohammed Iqbal Dar nae aliondoka nchini mwaka 1965 na kwenda kuishi Uingereza. Hakukata uhusiano hata kidogo na nchi alikozaliwa. Nyumba yake huko Birmingham Uingereza aliipa jina 'Dar es salaam' kwa heshima ya mji maarufu wa kibiashara Tanzania. Mwaka 2003 alikuja Tanzania kuhudhuria mkutano wa mwaka Jalsa Salana na toka wakati huo kila mara ilipopatikana fursa alihudhuria mikutano ya mwaka. Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alisema; 'Pelekeaneni zawadi mpendane'. Agizo hili alilishika vilivyo bw. Mohammed Iqbal Dar. Kila alipopata fursa ya kutembelea Tanzania hakukosa kubeba zawadi kwa Watanzania.

Ukurasa 04

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenziya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE










MAISHA YA MOHAMED IQBAL DAR (1944 – 2025)

Na Mahmood Hamsin Mubiru

MASOMO NA KAZI


Alikuwa ni hodari,
Mohammad Bin Dari,
Akasifiwa vizuri,
Wanafunzi na Walimu.

Aling'ara darasani,
Hata huko michezoni,
Jinale pale shuleni,
Wote wakalifahamu.



Mohamed Iqbal Dar mwana wa Daktari maarufu Tufail Ahmad Dar, alizaliwa mji ulio kandokando ya bahari ya Hindi – Tanga tarehe 08/08/1944. Baba yake aliyekuwa Daktari katika mashamba ya mkonge alihamia Morogoro na kuanzisha hospitali yake. Hivyo Mohamed Iqbal Dar alianza masomo yake ya shule ya msingi H. H. The Agakhan tarehe 01/04/1954 na baadae kujiunga na Secondari hapo hapo H. H. The Agakhan hadi tarehe 30/12/1962. Akiwa shule ya Secondari H. H. The Agakhan alikuwa kiranja wa shule na kipindi chake hicho alifanya kazi iliyomzolea sifa. Mwaka 1961 alipewa zawadi ya kuwa Kiranja bora hapo shuleni. Toka 1961 hadi 1962 alikuwa katika timu ya mpira wa magongo. 1962 alikuwa Kapteni wa timu ya mpira wa magongo iliyoshirikisha shule zote za H. H. The Agakhan Afrika Mashariki na timu aliyoiongoza iliibuka mshindi. Alikuwa pia mahiri katika mchezo wa mpira wa kikapu, kukimbia, mpira wa miguu na mpira wa wavu (volleyball). Alikuwa mjumbe wa kamati ya Maktaba ya shule na Katibu wa Umoja wa kukusanya Stempu. Toka mwaka 1963 hadi 1964 alikuwa shule ya Mzumbe Secondary ambako aliendelea kushiriki katika uongozi wa Maktaba. Ni katika shule hii ndipo harakati za kubuni jina Tanzania zilipofanyika. Harakati hizi zimeelezwa kinaga

UK. 11



Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 5,000/=.

Je, Wajua?

wajua kuwa ili uone kitu, basi mwanga unaotoka katika kile kitu unatakiwa uwe umefika machoko. Mwanga wa jua unatumia dakika nane kufika duniani. Mwanga wa nyota unachukua miaka milioni kadhaa kufika duniani. Hivyo uonapo nyota, fahamu kwamba unachokiona hasa ni mwanga uliotoka katika nyota miaka milioni iliyopita, na unafika katika macho yako muda huo unaoangalia. Unachokiona sio sasa, unaona historia. Wanasayansi wanatumia historia hiyo kujua dunia iliumbwaje.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com